Toleo Na. 1 Machi 1, 2025

WIZARA YA AFYA

HOSPITALI YA BENJAMIN MKAPA





# TOLEO MAALUMU

## MIAKA MINNE YA MAPINDUZI YA HUDUMA ZA UBINGWA WA JUU BMH

4

#Kazi Iendelee.

# Yaliyomo




Mafanikio kwa Ujumla ........................................ 3
Utangulizi ........................................ 4
Kalam ya Mkurugenzi Mtendaji ........................................ 5
Idara ya Magonjwa ya Figo (Nephrology and Kidney Transplant) ........................................ 6
Idara ya Mfumo wa Mkojo (Urology) ........................................ 9
Idara ya Magonjwa ya Macho (Ophthalmology) ........................................ 11
Idara ya Magonjwa ya Damu (Hematology and Bone Marrow Transplant) ........................................ 12
Idara ya Magonjwa ya Moyo (Cardiology and Cardiothoracic Surgery) ........................................ 16
Idara ya Upasuaji Mifupa (Orthopaedic) ........................................ 19
Idara ya Magonjwa ya Saratani (Oncology) ........................................ 21
Idara ya Magonjwa ya Kinywa na Meno (Dentistry) ........................................ 23
Idara ya Magonjwa ya Wanawake na Afya ya Uzazi
(Obstetrics and Gynaecology) ........................................ 24
Idara ya Magonjwa ya Ndani na Mfumo wa Chakula
(Internal Medicine and Gastroenterology) ........................................ 25
Idara ya Maabara na Patholojia (Laboratory and Pathology) ........................................ 27
Idara ya Famasi (Pharmacy) ........................................ 29
Huduma Mkoba na Tiba Utalii (Outreach Services and Medical Tourism) ........................................ 31
Idara ya TEHAMA (ICT) ........................................ 33
Mradi wa Mtambo wa Oxygen (Oxygen Plant) ........................................ 35




# Mafanikio kwa UJUMLA



**Katika kipindi cha miaka 4 iliyopita tumefanikiwa kuboresha huduma bora kwa wagonjwa katika maeneo yafuatayo; kupunguza muda wa kusubiri huduma kutoka masaa 7 hadi masaa 4 tangu kuhudumiwa mpaka kuondoka, kupunguza malalamiko ya wateja kutoka asilimia 32 hadi asilimia 2.**

Tumefanikiwa kuongeza wagonjwa wa nje (OPD) kutoka wagonjwa 700 hadi wagonjwa 1200 kwa siku, Wagonjwa wa kulazwa pia wameongezeka kutoka 120 hadi 294 kwa siku.

Tumefanikiwa kuimarisha huduma za kliniki maalumu ya viongozi. Kwasasa wagonjwa wanaofika hiyo kwa siku ni wagonjwa 40 ukilinganisha na wagonjwa 18 ambao walikuwa wakihudumiwa kipindi cha nyuma.

Huduma za VIP na Private zimeboreshwa na vyumba vimeongezeka kutoka 30 hadi kufikia 42.

Wagonjwa wanaolazwa VIP/PRIVATE kwa siku wameongezeka kutoka 15 hadi 38 kwa siku.

Huduma kwa mteja zimeimarishwa kwa kuweka mifumo mbalimbali kama vile Call center, Niulize mimi, dawati la malalamiko, jukwaa la mitandao ya kijamii, ujumbe wa jumla kwa wateja (bulk message), makundi sogozi kuhusiana na matibabu pamoja na mafunzo ya huduma kwa mteja

Pia kitengo cha huduma kwa mteja kinapata wateja wengi wanaokuja kujifunza namna ya kutoa huduma kwa wateja na kuwajengea uwezo watumishi toka maeneo mbalimbali nchini, ukilinganisha na miaka 4 nyuma ambapo kitengo hicho hakikuwa na uwezo wa kutoa mafunzo hayo.





# Utangulizi



Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) ni hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kati iliyozinduliwa na Rais wa Awamu ya Nne na Mheshimiwa Jakaya Kikwete tarehe 13 Oktoba, 2015. BMH ilianzishwa kwa ajili ya kuhudumia wananchi milioni 14 kutoka Kanda ya Kati na mikoa 7 ya jirani. Kwa siku inahudumia wananchi 1000 mpaka 1200. Mwaka 2025 inafikisha muongo mmoja wa huduma.

Ikiwa na vitanda 400 mbavyo uwezo wake unatarajia kuongezeka mpaka vitanda 600 mwisho wa mwaka 2025, BMH inatoa huduma 16 za ubingwa wa juu ambazo ni matibabu ya mfumo wa chakula (gastroenterology), upasuaji wa matundu madogo (laparoscopic and endoscopic surgery) upasuaji wa ubongo na mfumo wa fahamu (neurosurgery), upasuaji wa uti wa mgongo (spinal surgery). Matibabu ya magonjwa ya figo (nephrology), ikiwemo kuchuja damu (hemodialysis), upandikizaji figo, Matibabu ya amagonjwabya damu ikiwemo upandikizaji uloto. Matibabu mengine ni pamoja upasuaji wa kubadilisha nyonga na magoti (hip and knee replacement), matibabu ya magonjwa ya moyo, uchunguzi na matibabu ya mishipa ya moyo kwa kutumia vifaa vya kisasa kwenye maabara maalumu ya moyo (catheterization lab) upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua (cardiothoracic surgery), upasuaji wa mishipa ya damu (cardiovascular surgery), uchunguzi na matibabu ya kiradiolojia (intervention radiology), uvunjaji wa mawe kwenye mfumo wa mkojo kwa kutumia mawimbi (external shock wave and laser lithotripsy) upandikizaji uume (penile implantation).

## Mafanikio 15 makubwa katika miaka 10 ya huduma

**1.** Huduma bora na zenye kutumia teknolojia ya kisasa

**2.** Huduma za ubingwa wa juu kama upandikizaji figo (wagonjwa 50 kwa gharama ya Tsh B 1.65 nchini ambapo ingetolewa rufaa nje ya nchi Serikali ingetumia Tsh b 3.25 hivyo kuokoa Tsh b 1. 6. Upandikizaji uloto kwa wagonjwa 20 (kwa gharama ya Tsh 1.32 ikilinganishwa na Tsh B1.8 na kuokoa Tsh m 450) upasuaji wa ubongo na mifupa, upasuaji koo, pua, masikio, macho na kusafisha figo.

**3.** Kuanzisha huduma ya upasuaji wa kisasa wa matundu kwa wagonjwa wenye mawe kwenye figo na njia ya mkojo(Laparoscopic and Endoscopic surgery).

**4.** Upanuzi wa miundombinu ya huduma kwa kutekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la tiba za saratani ikiwemo mionzi (nuclear medicine na kansa wenye thamani ya Tsh B 30.9

**5.** Kusimika na kuendesha mtambo wa kuzalisha hewa ya Oxygen wenye uwezo wa kuzalisha mitungi 400 kwa siku((Oxygen plant).

**6.** Kuongeza idadi ya watumishi kutoka 22 hospitali ilipoanzishwa mpaka kufikia 967 (kwa mwaka 2024) na kuwaendeleza kwa kuwapa mafunzo.

**7.** Kununua vifaa vya kisasa vya uchunguzi kama CT Scan, MRI na vya maabara ya kawaida na maabara ya moyo (cath lab).

**8.** Kuanzisha chuo cha mafunzo ya Diploma za afya na kituo cha mafunzo ya huduma ya dharura (emergency medicine and critical care skills lab)

**9.** Kuanzisha huduma za ubingwa wa juu za dharura na wagonjwa mahututi wa kawaida.

**10.** Kutoa huduma za kibingwa mkoba na tembezi katika mikoa na maeneo ya pembezoni

**11.** Kufanya tafiti za tiba kwa kushirikiana na taasisi zingine.

**12.** Kupanua mashirikiano na wadau, ndani na nje ya nchi

**13.** Kuimarisha mawasiliano ya umma na utoaji wa elimu ya kinga na magonjwa kwa wananchi.

**14.** Kuimarisha uwezo wa taasisi kifedha kuweza kununua dawa (upatikanaji dawa sasa 90-95% toka 30% mwaka 2016) vitendanishi na vifaa tiba

**15.** Kupunguza rufaa kwa wagonjwa kwenda kutibiwa nje ya Hospitali kwa 85%

# Kalamu ya Mkurugenzi Mtendaji



Ndugu msomaji,

**Karibu kwenye jarida maalumu la mafanikio ya Hospitali ya Benjamin Mkapa, toleo maalumu ambalo linaangazia mafanikio tuliyopata Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) katika miaka minne (4) ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano.**

Kwa kipindi cha miaka miaka 4, huduma za ubingwa wa juu tunazotoa hapa Hospitalini zimeongezeka kutoka 7 mpaka kufikia 16. Haya ni mafanikio makubwa katika sekta yetu ya Afya kwani hii imeendelea kupunguza rufaa za nje ya nchi.

Mwezi Machi mwaka huu, tumekuwa Hospitali ya kwanza ya Serikali kufanya upasuaji kwa kutumia teknolojia ya mawimbi ya sauti kitaalamu High Intensity Focused Ultrasound (HIFU) tulipomtolea mgonjwa uvimbe wa ubongo.

Kwa miaka minne (4) iliyopita, jumla ya wagonjwa 1,061 wamepatiwa huduma za upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu na ubadilishaji nyonga na magoti. Kati yao 771 wamefanyiwa upasuaji wa ubongo wa ubongo na 290 upasuaji wa uti wa mgongo.

Mpaka sasa, tumefikisha watoto ishirini (20) kuwatibu ugonjwa wa sikoseli toka tulipozindua huduma hii Mei, 2023, matibabu haya tunayotoa kwa kufanya upandikizaji uloto. Watoto wote hawa ishirini wamenufaika kugharamiwa matibabu na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kupitia huduma za tiba za kibingwa na ubingwa wa juu, tunajukumu la kuwahudumia Wananchi milioni 10 katika mikoa saba ya kanda ya kati na mikoa jirani.

**Prof Abel N. Makubi**
**Mkurugenzi Mtendaji**



# Idara ya Magonjwa ya FIGO

## (Nephrology and Kidney Transplant)




**Utangulizi**

Idara ya tiba za magonjwa ya figo ya Hospitali ya Benjamin Mkapa inatoa huduma za uchunguzi na matibabu kwa watu wenye magonjwa ya figo. Huduma hizi hutolewa katika kliniki maalum ya magonjwa wa figo, huduma ya kuchuja damu, huduma ya wagonjwa waliolazwa na huduma ya upandikizaji figo. Idara hii ilianzishwa mwaka 2018

Huduma mbali mbali zilizotolewa kati ya mwaka 2021 na Januari 2025 ni kama zinavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.

**Huduma zinazotolewa katika idara ya figo ni kama ifuatavyo:**

1. Kliniki ya wagonjwa wa figo
2. Huduma ya uchujaji wad amu (hemodialysis)
3. Huduma kwa wagonjwa wanaohitaji kulazwa
4. Huduma ya upandikizaji figo

Kliniki ya figo inahudumia wastani wa wagonjwa 25-35 kwa siku, Kitengo cha kuchuja damu (hemodialysis) kinahudumia wastani wa wagonjwa 35-45 kwa siku, Idara inapokea wagonjwa wapya wanaohitaji kulazwa 1-2 kwa siku, Idara ya figo imefanikiwa kuanza na kuendelea kutoa matibabu ya upandikizaji figo ambayo inahitajika kwa Watanzania wengi walilazimika Kwenda nje ya nchi. Mpaka 2025 jumla ya wagonjwa 50 wamefanyiwa upandikizaji figo.



***Dkt. Sabina Mbali***
*Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Figo*

| Mwaka | Mahudhurio ya kliniki ya figo | Mahudhurio ya uchujaji damu (hemodialysis | Huduma ya upandikizaji figo |
|---|---|---|---|
| 2021-2022 | 1,202 | 14,436 | 9 |
| 2022-2023 | 1,893 | 15,353 | 6 |
| 2023-2024 | 2,379 | 9,741 | 5 |
| 2024-2025 | 2,293 | 5,687 | 9 |
| Jumla | 7,766 | 45,217 | 29 |

# Idara ya Magonjwa ya FIGO
## (Nephrology and Kidney Transplant)

4

**Uwekezaji wa Serikali na Wadau katika idara.**

1. Idara inatekeleza mradi wa Ujenzi wa vyumba jumuishi vya kutolea huduma za upandikizaji figo ambao umefikia asilimia 80.
2. Kusomesha wataalam wa kada mbali mbali wakiwemo madaktari bingwa na madaktari bingwa bobezi kwa ushirikiano wa serikali na wadau wa maendeleo
3. Ufadhili wa serikali wa wagonjwa 10 wenye uwezo mdogo wa kugharamia matibabu ya upandikizaji figo kwa kiasi cha tsh. 350,000,000/-
4. Idara iko kwenye mchakato wa Ujenzi wa kituo cha umahiri cha upandikizaji wa viungo ambao unafanyika kwa ushirikiano na Shirika la Tokushukai medical group la nchini Japan na Chuo Kikuu cha Dodoma. Hatua iliyofikia kwa sasa ni upembuzi yakinifu na usanifu wa majengo. Kituo hiki kikikamilika kitaongeza sehemu kwa ajili ya mafunzo, utafiti na kutanua eneo la kutolea huduma za upandikizaji kwa watu wa Afrika Mashariki na Kati.

Idara ina watumishi wafuatao: Dkt. Sabina Matulo Mmbali (Msc. Nephrology) Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Figo, Dkt. Kessy Charles Shija (Msc. Nephrology), Daktari bingwa (internal medicine Physician) 1, Daktari 1, Wauguzi 9, Afisa lishe 2, Wahudumu wa afya 3.




# Idara ya Magonjwa ya FIGO
**(Nephrology and Kidney Transplant)**





## Patient Survival Rate

***Figure 1: Graph:***
*Show the patient's survival rates at 1, 3, and 5 years which were 98.5%, 90% and 85.5% respectively.*




## Patient Survival Rate

***Figure 2: Graph***
*Show the survival rates at 1, 3, and 5 years which were 90%, 85% and 83% respectively.*



# Idara ya Mfumo wa MKOJO
**(Urology)**



**Idara ya tUrology ilianzishwa mwaka 2015 wakati hospitali ilipoanzishwa ikiwa na daktari bingwa mmoja na baada ya miaka 10 ina madaktari bingwa 7.**

Huduma zinazotolewa ni; Kliniki (matibabu ya nje), Kulaza wagonjwa na Upasuaji katika Mfumo wote wa Mkojo (Figo, Mirija ya figo, Kibofu na njia ya mkojo),Tezi dume, jinsia ya kiume, mabusha, korodani) pamoja na upandikizaji wa figo na kuweka vipandikizi kwenye uume pamoja na Huduma za saratani ya tezi dume.

Huduma za kibobezi zilizoongezeka ni pamoja na kuweka vipandikizi katika uume kwenye wagonjwa 12, Kuanzisha huduma za kusaga mawe kwenye mfumo wa mkojo kwa kutumia miale(laser lithotripsy) tangu mwaka 2021 na mpaka sasa tumehudumia wagonjwa 147.

Mafunzo na Matibabu: Idara imefanikiwa kufanya matibabu na mafunzo mbalimbali ndani ya hospitali na ndani ya nchi.


Mipango ya siku zijazo: Ni kuanzisha taasisi yaani Institute of Urology, itakayokuwa ikitoa tiba jumuishi za magonjwa ya mfumo wa mkojo kwa aina zake, kufundisha wataalamu wa tiba za mfumo wa mkojo na kufanya tafiti na majaribio ya kisayansi ya tiba za kisasa za magonjwa ya Mfumo wa Mkojo.

**Orodha ya wataalam katika Idara.**

Idara inaongozwa na Dkt. Remigius A. Rugakingira (Superspecialist), Dkt. Okoa Sukunala, MD, Mmed(Urol), Dkt. Vitus Kajerero, MD, Mmed(urol), Dkt. Said Mawji MD, Mmed(Urol), Dkt. Reuben Mkinga, MD, MMed(Urol), Dkt. Dennis Kanyika, MD, Mmed(Urol), Dkt. Fredrick Mabena, MD, Mmed(Urol), Dkt. Elam Yango, MD, Dkt. Emmanuel A. Tairo, MD, Dr Anatory Prudence Alibalio, MD. Madaktari hawa wanafanya kazi kwa kusaidiana na wauguzi na wataalamu wengine.




***Dkt. Remigius A. Rugakingira***
*Mkuu wa Idara ya Mfumo wa Mkojo*



# Idara ya Mfumo wa MKOJO
## (Urology)



**Patient-Centered Care and Increased Demand**

The impact of these initiatives is evident in the rising number of patients seeking care at BMH- Urology Department; In five years (2018-2023) a total number of 65,523 [14] clients were attended and cared. The clinic evolved from two days a week to five days in a week, the department now operates clinics throughout the workweek.

Figures 1 and 2 below provide details of the number of patients that were given urological services at Benjamin Mkapa Hospital.





***Figure 1:*** *Age and Sex distribution for patients attended at BMH Urology Department*





***Figure 2:*** *Male and Female ratio of patients who attended at Urology Department*

# Idara ya Magonjwa ya MACHO
## (Ophthalmology)



**Idara ilianzishwa mwaka 2015 pindi Hospitali ilipoanzishwa na ilikuwa na Daktari Bingwa mmoja (Specialist) na wauguzi wawili huku idadi ya wagonjwa wakiwa watatu kwa siku.**

**Idara inatoa huduma zifuatazo:**

1. Uchunguzi wa kibingwa
2. Huduma za Upasuaji
3. Huduma za Miwani(Optometria)
4. Huduma za Kliniki mkoba (outreach services)
5. Mionzi kwenye Macho

Mwenendo Idadi wa idadi ya Wagonjwa ambao wamekuwa wakihudumiwa katika idara ya macho imekuwa ikiongezeka siku hadi siku, kwasasa tunahudumia wastani wa wagonjwa 850 kwa Mwezi.

**Mafanikio ya Idara:**

1. Tumeanzisha Karakana ya Miwani.
2. Tumenunua mashine za kisasa kama mashine ya mionzi,
3. Ultrasound ya macho, Visual Field, IOCT.
4. Kufanya operation za Kibingwa kama kutoa mtoto wa jicho kwa tundu dogo.
5. Ukarabati wa sehemu mbalimbali za macho.
6. Uwekezaji wa Serikali na Wadau katika idara.
7. Kuongeza watumishi (BMH)
8. Ukarabati wa vyumba vya upasuaji (BMH)
9. Mashine na vifaa mbalimbali (BMH na IFW)
10. Mafunzo kwa watumishi mbalimbli

**Mipango ya siku za mbele/siku za usoni**

Idara inatarajia Kuongeza huduma za kibingwa bobezi. Kuwa na kituo cha umahiri cha tiba za macho, Kuimarisha Ushirikiano na wadau tofauti ndani nan je ya nchi na Kuimarisha Mafunzo na Maendeleo ya Kitaaluma

**Watumishi waliopo:** Mkuu wa idara, Dr. Jacinta M. Feksi, Daktari bingwa bobezi:Dr. Amon Kyando Mwakakonyole (Paediatric Ophthalmologist), Dr.Frank Albert Sandi (Glaucoma Specialist) Wataalamu wengine katika idara ni Madaktari Bingwa macho: Dkt. Joshua Youze, Dkt.Sophia Gomba (UDOM), Dkt. Majula Mganga. **Madaktari wa kawaida:** Dkt. Salma Bentas, Dkt. Sonia Luhindi. Optometria: Opt. Godfrey Felix, Opt. George Mwikola, Opt. Sigfrid Shirima, Opt. Ally Mohamed na Wauguzi wa macho: 6



***Dkt. Jacinta M. Feksi***
***Daktari bingwa Bobezi,*** *Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Macho*

# Idara ya Magonjwa ya DAMU

## (Hematology and Bone Marrow Transplant)



**Utangulizi:**

Idara ya tiba za magonjwa ya damu(hematolojia) ilianzishwa mwaka 2018 ikihudumia wagonjwa wa damu kutoka mikoa ya Kanda ya Kati (Dodoma, Singida, Manyara, Iringa na Tabora).

**Huduma zinazotolewa na idara ya Magonjwa ya Damu:**

Idara inatoa elimu ya magonjwa ya damu (Health Education), inafanya uchunguzi wa awali wa magonjwa ya damu kama Sikoseli, Hemofilia, na kutoa matibabu ya kibingwa na Bingwa bobezi ya matibabu ya magonjwa ya damu yanayojumuisha

- Upandikizaji Uloto (BMT)
- Huduma za damu salama za kibingwa na ubingwa bobezi (Kusafisha damu (Red Cell Exchange), Apheretic plataelets, Irradiated/Leucofiltered blood products, Extended blood grouping and crossbmatching))

Idadi ya wagonjwa waliopatiwa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi: Kati ya mwaka 2021-2025 wagonjwa wamepatiwa matibabu mbalimbali kupitia idara ya magonjwa ya damu Wanaohudumiwa katika idara – (Outpatiens, Inpatients)

1. Upandikizaji Uloto (Bone Marrow transplant, BMT) Watoto 20 wenye ugonjwa wa selimundu wamepatiwa matibabu haya kwa mafanikio makubwa na wote wanaendelea vizuri kati ya mwaka 2023-2025
2. Huduma za juu za Damu Salama (Automated Red Cell Exchange) Wagonjwa 30 wenye sikoseli wamepatiwa huduma ya ushafishaji damu na hivyo kupunguza ukali wa ugonjwa wa sikoseli.
3. Upandikizaji Uloto (Bone Marrow transplant, BMT) Watoto 20 wenye ugonjwa wa selimundu wamepatiwa matibabu haya kwa mafanikio makubwa na wote wanaendelea vizuri kati ya mwaka 2023-2025.
4. Matibabu ya Hemofilia (factor replacement therapy) Wagonjwa 33 wa hemofilia wametambulika na kuanzishiwa matibabu.

**Mafanikio mengine**

Idara imeanzisha huduma ya upandikizaji uloto na kuifanya Tanzania kuwa moja ya nchi sita barani Afrika zinazotoa huduma hii (watoto 20 wenye sikoseli wamepandikizwa uloto), Kunzisha huduma za juu za damu salama (Apheretic



***Dkt. Stella Malangahe***
*Mkuu wa Idara ya Hematolojia*

# Idara ya Magonjwa ya DAMU
**(Hematology and Bone Marrow Transplant)**



4

## Bilioni 2.7
**Kiasi cha fedha kilichotumika kuanzisha huduma ya upandikizaji uloto**

procedures, irradiation of blood, leucofiltration), kuanzisha huduma za matibabu ya himofilia kwa wagonjwa wa kanda ya kati

Uwekezaji wa Serikali na Wadau katika idara – Miundombinu, Mashine na Vifaa Tiba, Rasilimali Watu na Mafunzo

**Uboreshaji wa miundombinu**

Jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 2.7 kilitumika kuanzisha huduma ya upandikizaji uloto.

Fedha hizi zilitumika katika, mafunzo kwa watumishi 10 wa kitengo cha upandikizaji uloto (madaktari, wauguzi, wataalam wa maabara na wahandisi), ukarabati wa wodi ya upandikizaji uloto, ununuzi wa madawa, vitendanishi na vifaa tiba, na uboreshaji wa baadhi za huduma za maabara, famasi na damu salama.

**Gharama za upandikizaji uloto**

Jumla ya shilingi bilioni 1.1 ziliwasilishwa BMH kwa ajili ya kugharamia upandikizaji uloto kwa watoto 20 wenye sikoseli, ambapo serikali imeokoa kiasi cha shilingi milioni 500 ambacho kingetumika endapo wagonjwa hawa wangepatiwa upandikizaji nje ya nchi.

## Bilioni 1.1
**Kiasi cha fedha kilichowasilishwa BMH kwa ajili ya kugharamia upandikizaji uloto kwa watoto 20 wenye sikoseli**

**Mipango ya siku za mbele**

Kuanzisha kituo cha umahiri cha upandikizaji uloto na sayansi ya magonjwa ya damu cha Afrika mashariki, Kuongeza wigo wa huduma ya upandikizaji uloto kwa magonjwa mengine ya damu kama Aplastic Anemia na saratani za damu, na kupatia mafunzo timu ya wataalam watakao bobea katika huduma mbalimbali za utoaji huduma za magonjwa ya damu

Watumishi wa Idara: Dkt Stella Malangahe, Daktari Bingwa magonjwa ya damu na Wataalamu wengine katika idara ni Madaktari Bingwa: Dkt. Irene Mteta, Dkt. Catherine Muhando, Dkt. Happiness Igogo, Madaktari wa kawaida: Dkt. David Mashalla, Dkt. William Lyodd na Dkt Julieth Obeid

# Idara ya Magonjwa ya DAMU
## (Hematology and Bone Marrow Transplant)








# Idara ya Magonjwa ya DAMU
## (Hematology and Bone Marrow Transplant)



4






# Idara ya Magonjwa ya MOYO
## (Cardiology and Cardiothoracic Surgery)




**Katika kipindi cha miaka minne BMH imefanya upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua kwa wagonjwa 60 kati ya hao watoto 38 na watu wazima 22. Kiasi cha fedha kilichotumika katika upasuaji huu ni millioni 562 na kati ya hizo millioni 100 zilitoka mfuko maalum wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan.**

Aidha wataalamu wetu wamefanya uchunguzi wa mishipa ya moyo (Cardiac Catheterization) kwa wagonjwa 1173, upandikizaji betri kwa wagonjwa 23, kuweka vizibua njia ya mishipa ya moyo (Stents) kwa wagonjwa 200.

**Mipango ya baadaye**

Kujenga Hospitali ya Moyo ya kuhudumia watoto na watu wazima wenye matatizo ya moyo. Kuanzisha mfuko wa kusaidia matibabu ya moyo kwa watoto wasiokuwa na uwezo.




**Dkt. John Meda**
*Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Moyo*



# Idara ya Magonjwa ya MOYO
## (Cardiology and Cardiothoracic Surgery)





# Idara ya Magonjwa ya MOYO

## (Cardiology and Cardiothoracic Surgery)



***Figure 1:*** *Number of adult cardiac catheterization procedures performed from 2019 to 2024respectively.*






***Figure 2:*** *Number of pediatric cardiac catheterization procedures performed from 2019 to 2024*



# Idara ya Upasuaji wa MIFUPA
## (Orthopaedic)



Mafanikio mengine ni pamoja na Upasuaji wa Ubongo na mishipa ya fahamu ambapo katika miaka minne, jumla ya wagonjwa 1061 walifanyiwa upasuaji. Kati yao, 771 walifanyiwa upasuaji wa ubongo na 290 walifanyiwa upasuaji wa uti wa mgongo. Aidha, wagonjwa 440 wamebadilishiwa nyonga na magoti, wagonjwa hawa wangepata huduma nje ya nchi ingegharimu kiasi cha shilingi Bilioni 8.8, kwa kupata huduma katika Hospitali ya Benjamin Mkapa imegharimu shilingi bilioni 2.3 hivyo serikali imeokoa shilingi bilioni 6.5

**Malengo ya baadaye**

1. Kuendelea kuongeza idadi ya wagonjwa wa upasuaji wa kubadilisha nyonga, goti na pia upasuaji wa mivunjiko ya nyonga na Upasuaji wa goti kwa kutumia matundu madogo kwa asilimia thelathini (30%) kwa kila aina ya upasuaji.
2. Kuendelea kutangaza upatikanaji wa huduma hizi katika Hospitali yetu
3. Kufanya kambi maalumu mara moja kwa mwaka kwa kila aina ya upasuaji kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi
4. Kuongeza ujuzi wa wataalamu wa ndani ili kuwajengea uwezo wataalamu hawa kwa kushiriki mikutano ya kitaaluma na kozi fupi za ndani na nje ya nchi.



**Dkt. Mike Chacha**
*Mkuu wa Idara ya Upasuaji wa Mifupa*



# Idara ya Upasuaji wa MIFUPA
## (Orthopaedic)







# Idara ya Magonjwa ya SARATANI
## (Oncology)



**Idara ya saratani ilianzishwa mwaka 2018 ikiwahudumia wagonjwa wa saratani mkoani Dodoma na mikoa ya kanda ya kati. Huduma zinazotolewa na idara (tangu Ilipoanza na sasa): Utoaji wa elimu ya saratani (Health Education), kufanya uchunguzi wa saratani (Cancer Screening), Kutoa matibabu ya saratani kwa kutumia tiba kemotherapia (Chemotherapy) na Tiba Shufaa (palliative care).**

Mwenendo wa Wagonjwa ambao wamekuwa wakihudumiwa katika idara – (Outpatiens, Inpatients): Kati ya mwaka 2021-2025 wagonjwa 13,000 (wanawake 7,183 na wanamue 5,342) walihudumiwa kama wagonjwa wa ndani na wa nje.

**Mafanikio ya Idara:**

1. Wagonjwa takribani 13,000 waliogundulika na Saratani wamepatiwa matibabu, Upatikanaji wa dawa za saratani kwa zaidi ya asilimia 90 kwaajili ya saratani za aina mbali mbali,
2. Vifaa vya ugunduzi wa saratani vya kisasa kama Mammaography na Colonoscopy kupatikana kwaajili ya uchunguzi wa saratani,
3. Kuwa na mtambo wa Kisasa wa kuchanganjia dawa (compounding machine),
4. Mradi mkubwa wa ujenzi wa Jengo la matibabu ya saratani umefikia





**Dkt. Jesse Kashabano**
*Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Saratani*

# Idara ya Magonjwa ya SARATANI
## (Oncology)

asilimia 57. Jengo hilo pia litakua kituo cha umahiri wa utoaji huduma za saratani na tafiti Africa,

5. Serikali imeendelea kusomesha madaktari, wauguzi, wafizikia katika eneo la saratani ambapo hadi sasa wataalamu takribani 15 wapo katika mafunzo mbalimbali.

Uwekezaji wa Serikali na wadau katika idara – miundombinu, mashine na vifaa tiba, rasilimali watu na mafunzo: Ujenzi wa jengo jipya la matibabu ya saratani ambalo litagharimu bilioni 32, mpango wa ununuzi wa machine za mionzi (radiotherapy machine) na mashine za tiba ya nuklia (nuclear medicine), kuongeza idadi ya watalaamu hadi sasa si chini ya wataalamu 15 wanaoendelezwa katika huduma za saratani ikiwa ni hatua ya kuendelea kuboresha huduma za saratani.

**Mipango ya siku za baadaye:**

Kuwa kituo namba moja Tanzania katika utoaji wa huduma jumuishi za saratani, Kutoa huduma za Mionzi kwa kutumia machine mpya na za kisasa ukilinganisha na sehemu nyingine zinazotoa mionzi, Kuwa kituo cha umahiri katika kutoa huduma za saratani na utafiti, Kutoa matibabu kwa kutumia nuklia katika hatua zote za ugunduzi hadi matibabu ( Nuclear medicine ), Kuwa kituo bora katika utoaji wa tiba Shufwaa (palliative care) kwa wagonjwa wenye saratani na maradhi mengine ya muda mrefu, Kuhudumia wateja wengi zaidi wa ndani na nje ya nchi na Kufundisha madaktari bingwa bobezi
wa upasuaji wa saratani kufikia mwaka 2030

Watumishi wa Idara: Mkuu wa Idara JESSE JONATHAN KASHABANO, Daktari Bingwa magonjwa ya saratani (Clinical Oncologist) na Mtafiti wa masuala ya saratani. Wataalamu wengine katika idara ni Dkt. Ramadhan Senga, Dkt. Annetha Clement na Wauguzi: Florah Njiku ( Muuguzi wa saratani (Msc nursing oncology), Suzana Peter (NO), Sr. Shukrani.



# Idara ya Magonjwa ya KINYWA na MENO
**(Dentistry)**



Katika kipindi cha miaka minne Idara ya Kinywa na Meno imefanikiwa kuongeza huduma meno bandia kwa zaidi ya wagonjwa 200, kupanga meno (Orthodontic treatment) zaidi ya wagonjwa 240 wamepata huduma hii, Upasuaji mkubwa (Major operations) wananchi 20 wamepata huduma na kwa asilimia 90 wanaendelea vizuri, Mdomo sungura (Specialised Operations-cleft lips and palate) na (Crowns and bridges for teeth replacement. Mipango ya baadaye ni kuanzisha Vipandikizi vya meno (Teeth Implants), Meno bandia ya Ceramic ya kuvaa moja kwa moja (Ceramic crowns) na upasuaji wa meno na ufizi kwa wagonjwa wenye meno yaliyolegea kwa maradhi ya fizi ili kuimarisha kama awali (Periodontal Surgeries)





***Dkt. Alex Kimambo***
*Mkuu wa Idara ya Kinywa na Meno*

# Idara ya Magonjwa ya KIKE na Afya ya UZAZI
## (Obstetrics and Gynaecology)



**Katika Idara hii, tumefanikiwa kufungua chumba cha upasuaji wakina mama/wajawazito kinachotoa huduma za dharura.**

Tumefanikiwa pia kuanzisha huduma ya uzazi shirikishi ambao humpa mama kuchagua mtu mmoja ambaye atakuwepo na kushuhudia anapo jifungua.

Pia tumefanikiwa kupata vifaa kwa ajili ya uanzishaji wa huduma ya upandikizaji mimba na mbegu za kiume na sasa tunaelekea kumaliza ukarabati wa jengo.

Kupitia ufadhili wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania, madaktari wawili wameenda kusomea ubingwa bobezi wa upandikizaji wa mimba na mbegu za kiume.

Lakini pia tumeanzisha huduma za uchunguzi na upasuaji kwa njia ya matundu.



***Dkt. Israel Soko***
*Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Magonjwa ya Kike na Afya ya Uzazi*

## WATOTO:

**Mafanikio**

Tumefanikiwa kufanya yafuatao

1. tumeendelea kuboresha hududma za mtoto mchanga  kwa sasa Hopsital yetu imeweza kuhudumia watoto wanaozaliwa na 600-700gm
2. Tumeendelea kufanya uchunguzi na kutibu watoto wenye saratani mbalimbali kama vile saratani za damu, tezi, figo, neroblastoma na saratani za ubungo
3. tumeanzisha clinic za mfumo wa chakula kwa watoto,upumuaji , mkojo. mfumo wa fahamu
4. Tunafanya uchunguzi na kutibu watoto wenye matatizo ya magonjwa ya moyo.
5. tumeendelea kuongeza vifaa; ventilator, CPAP Machine, incubator, warmer, monitors, phototherapy machines n.k.

**Katika kuzuia magaonjwa**

Tumeanzisha kliniki ya 'well babay care' Inayofanya mambo yafuatayo

• Kufuatilia maendeleo na mwenendo wa makuzi ya mtoto

• Counseling feeding + breast feeding support to old and first time parents

• Screening for rare diseases like hearing loss, rare disease, nutrition problem.

# Idara ya Magonjwa ya NDANI na Mfumo wa CHAKULA

**(Internal Medicine and Gastroenterology)**



4

**Idara hii ni kiungo muhimu mno kwenye huduma za afya hapa hospitalini kwetu ambayo nimejikita katika kutoa huduma za uchunguzi, utambuzi tiba na kinga ta magonjwa kadhaa katika mwili wa mwanadamu. Idara inatoa huduma jumuishi kwa wagonjwa wenye maradhi ya aina zote hata maradhi sugu kwa kutumia njia za tiba za kisasa zilizothibitishwa kitaalamu.**

Idara ilianzishwa mwaka 2015 na kupanuka na kuanzisha huduma za ubobezi kweye eneo la tiba za magonjwa ya mfumo wa chakula (Medical Gastroenterology) mwaka 2019, Magonjwa ya Ngozi (Dermatology) Mwaka 2021 na Endocrinologia (Medical Endocrinology) Mwaka 2022.

**Orodha/idadi ya Huduma zinazotolewa na idara (Ilipoanza na sasa)**

- Huduma za kibingwa kwenye tiba za magonjwa (General specialized Internal Medicine Services)
- Huduma za ubobezi (Super specialized Medical Services) Kama vile
  – Magonjwa ya mfumo wa chakula na Ini(Gastroenterology and Hepatology)
  – Magonjwa ya kisukari na vichocgeo vya mwili (Endocrinology and Diabetes Care)
- Huduma nyingine ni:-
  – Magonjwa ya kuambukiza yaani Infectious Diseases (e.g. TB and HIV)
  – Huduma za uangalizi wa wagonjwa mahututi (Intensive Care Unit (ICU) and HDU services for critically ill patients)
  – Uchunguzi na upimaji (Diagnostic and Laboratory Services e.g. endoscopy, spirometry)
  – Elimu ya Afya (Health education on lifestyle diseases, nutrition, and physical activity)
  – Uchunguzi wa magonjwa kabla ya kuugua (Screening for diabetes, hypertension, cancer, and other chronic illnesses)
  – Huduma kwa wagonjwa wanaolazwa (Inpatient hospitalization for patients requiring close medical supervision)
  – Huduma za utafiti wa Magonjwa (Medical Research and Training)

**Mwenendo wa idadi ya Wagonjwa ambao wamekuwa wakihudumiwa katika idara – (Outpatients, Inpatients) 2020-2025**

- Idadi ya Inpatient
- Idadi ya Outpatient 130,511

**Mafanikio ya Idara**

Idara imefanikiwa kuanzisha huduma mpya

- Gastroenterology patients (10906)
- Dermatology patients (19127)
- Endocrinology – patients (11404)



***Dkt. Gloria Ngajilo*** *(Doctor of Medicine (MD), Mmed Internal medicine na MSc in Clinical Endocrinology) , Mkuu wa Idara.*

# Idara ya Magonjwa ya NDANI na Mfumo wa CHAKULA
## (Internal Medicine and Gastroenterology)



**Uwekezaji wa Serikali na Wadau katika idara – Miundombinu, Mashine na Vifaa Tiba, Human Resources na Mafunzo**

- Manunuzi ya vifaa vipya idarani kama spirometer
- Kwa kushirikiana na Idara ya Neurosurgery tulinunua mashine ya EEG,
- Wataalamu wapo masomoni.
- Mmed internal medicine – madaktari watano
- Msc Gastroenterology mmoja

**Mipango ya baadaye**

- Kuanzisha Kitengo cha Kiharusi
- Kuanzisha huduma za bronchoscopy
- Kuanzisha vipimo vya EMG and nerve conduction study
- Kuanzisha Multidisciplinary diabetic foot unit
- Kuboresha huduma za endoscopy kwa kuongeza huduma mpya za intervention kama ERCP, cryotherapy, Argon plasma photocoagulation
- Kuboresha huduma za dermatology kwa kuongeza huduma mpya za cosmetic dermatology, dermatosurgery, allergology,
- Kusomesha wataalamu kupata Ubingwa wa Juu mbalimbali kama vile neurology, infectious disease, pulmonology, rheumatology na allergology,

**Watumishi wa Idara:**

Mkuu wa idara ni Dkt. Gloria Ngajilo (Doctor of Medicine (MD), Mmed Internal medicine na MSc in Clinical Endocrinology).

Wataalamu wengine ni Dkt. Shani Budigoli - Dermatologist (MD, Mmed Dermatology), Dkt. Mastura Mutungi - Dermatologist (MD, Mmed Dermatology), Dkt. Emmanuel Sindato (MD, Mmed Internal Medicine, Msc Gastroenterology and Hepatology), Dkt. Lufunyo Lihweuli (MD, Mmed Endocrinology), Dkt. Happy Kassim (MD Mmed Internal Medicine), Dkt. Edwin Ochina (MD Mmed Internal Medicine), Dkt. Sophia Muhali (MD Mmed Internal Medicine), Idadi ya Wataalamu wengine katika idara, Medical officers 4.



# Idara ya MAABARA na PATHOLOJIA
**(Laboratory and Pathology)**



**Idara ya maabara inashughulika na utoaji wa huduma za kibingwa katika takribani vipimo zaidi ya miambili kwenye maeneo yafuatayo: Parasitology, Microbiology, Serology, Molecular Biology, Immunology, Clinical Chemistry, Haematology, Blood Transfusion na Histopathology kwa wagonjwa wa ndani na nje ya Benjamin Mkapa Hospital (BMH).**

Pia idara ina kitengo cha damu salama ambacho shughuli yake kuu ni kukusanya damu salama kwa ajili ya wangonjwa wenye uhitaji wa kuongezewa damu salama.

**Idadi ya Wataalamu katika Idara**

Idara ina Pathologist 3, Specialized Laboratory Scientist 2, Laboratory Scientist 16, Laboratory Technologist 38, Wauguzi 1, Laboratory Attendant 1, Social worker 1.

**Huduma zinazotolewa na Idara (ilipoanza na sasa)**

Tangu kuanzishwa kwake idara imeendelea kutoa huduma za upimaji wa sampling zilizoombwa wataalamu ili kuwasaidia kutoa matibabu stahiki kwa wagonjwa wote.



**_Dkt. Henry Stephen Joseph_**
*Mkurugenzi Msaidizi - Maabara*



# Idara ya MAABARA na PATHOLOJIA
**(Laboratory and Pathology)**



**Vipimi vya Maabara (2021-2024)**

| Section Name | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|
| BLOOD TRANSFUSION | 13752 | 15488 | 17852 | 18341 |
| CHEMISTRY | 85993 | 83432 | 110686 | 160781 |
| HAEMATOLOGY | 50094 | 50082 | 56683 | 69865 |
| HISTOLOGY | 2223 | 2708 | 2907 | 3248 |
| IMMUNOLOGY | 17077 | 15417 | 18448 | 24828 |
| MICRO BIOLOGY | 5271 | 7824 | 7998 | 9200 |
| MICRO TB | 802 | 1167 | 1125 | 1492 |
| MOLECULAR BIOLOGY | 0 | 0 | 4 | 4 |
| PARASITOLOGY | 51302 | 55399 | 58395 | 63472 |
| SEROLOGY | 21835 | 19522 | 24858 | 27347 |
| Grand Total | 248349 | 251039 | 298956 | 378578 |

**Mafanikio ya Idara**

i) Utafiti na Mafunzo

Idara imefanya publication mbili mwezi Machi 2022 zenye title "Antimicrobial Resistance Patterns of Escherichia coli O157:H7, Salmonella, and Shigella Species from Stool Samples of Patients with Diarrhea at Benjamin Mkapa Hospital" na tafiti nyingine yenye title "Prevalence, Antimicrobial Susceptibility Patterns of Bacterial Isolates and Risk Factors of Access Related Infection among Hemodialysis Patients at Benjamin Mkapa Hospital". Kadhalika, inaendelea na kuandaa data za "Antimicrobial Resistance Testing (AMR)" kwenye Kitengo cha Microbiology na kutuma data hizo maabara kuu ya taifa kama ilivyo azimio la Wizara ya Afya.

ii) Ithibati

Idara ya Maabara kutoa huduma katika kiwango cha kimataifa na kutunukiwa cheti cha ithibati. kutoka SADCAS baada ya kufanyiwa assessment mbalimbali

iii) Kuongeza vipimo

Idara imefanikiwa kuongeza vipimo mbalimbali katika idara mbalimbali frozen section, immunohistochemistry, histology, cytology, haematology, chemistry , Immunology.

# Idara ya FAMASI
**(Pharmacy)**





**Utangulizi**

Idara ya Famasi ilianzishwa Mwaka 2015, inatoa huduma za dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa wa nje na waliolazwa.

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KUANZIA MWAKA 2021-2024**

**1. Aina ya huduma**

Huduma zinazotolewa katika Idara ya Famasi zimeongezeka kutoka aina moja ya huduma iliyotolewa mwaka 2021 hadi kufikia aina tano za huduma. Huduma hizo ni:

1) Uchanganyaji wa dawa za wagonjwa ambazo hazipatikani sokoni (compounding);
2) Utoaji wa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa wa ndani na nje (in and outpatients);
3) Utoaji huduma kupitia Duka la Huduma za Dawa la Jamii (Community Pharmacy);
4) Uchanganyaji na utoaji wa dawa za kansa na za upandikizaji uloto; na
5) Utoaji wa taarifa na elimu kwa wagonjwa kukuza matumizi sahihi na usalama wa dawa;

**2. Maeneo ya kutoa huduma**

Maeneo ya kutolea huduma kwa wateja yameongezeka. Mwaka 2021 kulikuwa na maeneo mawili tu ya kutolea huduma za famasi na hadi mwaka 2024 maeneo hayo yameongezeka na kufikia 13. Maeneo hayo ni:


1) Main dispensing pharmacy;
2) Emergency Pharmacy;
3) Community Pharmacy;
4) Oncology Pharmacy;
5) Theater I Pharmacy;
6) Theater II Pharmacy;
7) Medicine Store;
8) Sub-store;
9) Drug Information Centre;
10) Inpatient Pharmacy;
11) Compounding Pharmacy;
12) CTC Pharmacy; na
13) Provision of field practical training to pharmaceutical students/ Kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa kada ya Famasi.





***Pharm. Emiliana Cosmas Bernado***
*Mkurugenzi Msaidizi - Famasi*

# Idara ya FAMASI
**(Pharmacy)**





3. **Idadi ya vyeti vya wagonjwa vilivyohudumiwa**

   Vyeti vilivyohudumiwa katika Idara ya Famasi imeongezeka, kutoka vyeti 131,106 mnamo mwaka 2021 hadi 222,197 mwaka 2024.

4. **Upatikanaji wa dawa**

   Kutoka na kuimarika kwa mnyororo wa ugavi wa bidhaa za afya unaosimamiwa na Idara ya Famasi, upatikanaji wa dawa umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka. Mwaka 2021 upatikanaji wa bidhaa za afya ulikuwa asilimia 80 na mwaka 2024 ulifikia asilimia 95.

5. **Watumishi wanaotua huduma za kifamasia**

   Idadi ya watumishi katika Idara imeongezeka kutoka 41 Mwaka 2021 hadi kufikia 68 mwaka 2024, ikiwa ni ongezeko la asilimia 60.29%

# Huduma MKOBA na Tiba UTALII

## (Outreach Services and Medical Tourism)



**Hospitali ya Benjamin Mkapa imekuwa ikitoa huduma mkoba katika mikoa ya Kanda ya Kati na Mikoa ya jirani ili kuwafikia Wananchi 18,000 wenye uhitaji na pia kuwajengea uwezo watuimishi katika maeneo hayo. Vilevile imeanzisha huduma mkoba maalumu kwa kutumia magari tembezi yenye vyumba vya upasuaji ambapo huduma hii imeanza kutolewa Zanzibar, Kondoa na sasa tunatarajia kwenda Burundi.**

Huduma za tiba utalii zimetolewa kwa wagonjwa wa DRC, Comoro na Oman.

**Mashirikiano**

Katika kipindi cha miaka minne Hospitali imekuwa na mashirikiano ya wadau wa ndani UDOM, Muhimbili, KCMC, na Bugando na wadau kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalamu wetu; Tokushukai Medical Group – Japan atika kujenga uwezo wa upadikizaji figo , Help 3 Monza –Italy-kujenga uwezo wa kupandikiza uloto, Pathology Without Boarder – Italy, Childrens Heart Charity Association – Kuwait, Zgt-Overzee Foundation – Netherland.






***Monica Kessy***
*Mkurugenzi wa Mafunzo, Utafiti na Ubunifu*

# Mradi wa Huduma MKOBA na Tiba UTALII

## (Outreach Services and Medical Tourism)

4





# Idara ya TEHAMA
## (ICT)

**1. Maboresho ya Huduma kwa Mteja kupitia Mifumo Mbalimbali**

**i. Mfumo wa Kupiga na Kupokea Simu (Call Centre)**

Hospitali imeanzisha mfumo huu kwa lengo la kurahisisha mawasiliano zaidi kati ya wagonjwa na watoa huduma wetu. Mfumo huu unawawezesha wagonjwa kupiga simu na kuuliza maswali mbalimbali kuhusu huduma zinazotolewa. Aidha, watoa huduma wa dawati la huduma kwa wateja hutumia mfumo huu kuwafikia wateja kwa simu, kuwajulia hali, na kuwakumbusha kuhusu miadi ya kurudi kliniki ili kuendelea na matibabu.

**ii. Matumizi ya simu za upepo (Radio calls)**

Hospitali inatumia simu za upepo katika kuimarisha mawasiliano kati ya watoa huduma, ili kuboresha ufanisi wa mawasiliano na kuongeza uwajibikaji kwa





**Bw. Gilbert William Chawe**
*Mkurugenzi wa TEHAMA na Takwimu*

# Idara ya TEHAMA
## (ICT)



watumishi. Simu hizi zinatumika na viongozi wote wa hospitali, hivyo taarifa zitawafikia watumishi kwa haraka na kusaidia kutatua changamoto kwa ufanisi zaidi.

**iii. Kuanzisha Fomu Maalum ya Kutoa Maoni kwa Njia ya Mtandao**

Hospitali pia imeanzisha fomu maalum ya mtandao inayowawezesha wateja kutoa maoni kuhusu huduma walizopokea. Mgonjwa anapata fursa ya kutoa maoni kuhusu huduma, watumishi waliomuhudumia, hali ya mazingira, na mambo mengine muhimu.

**iv. Kuanzisha Mfumo wa Ujumbe Mfupi (Bulk SMS)**

Hospitali imeanzisha mfumo wa kutuma ujumbe mfupi wa maneno (SMS) kwa lengo la kuwajulisha wagonjwa kuhusu majibu ya vipimo, miadi ya kliniki, na mambo mengine ya muhimu kuhusu huduma zao. Mfumo huu unasaidia kutoa taarifa kwa haraka na kwa urahisi na kufanya huduma kuwa shirikishi kwa mgonjwa.

**2. Kutumia Mfumo wa Kielektroniki katika Kumuona Mgonjwa (Integrated Health Management Information System)**

Hospitali inatumia mfumo wa kielektroniki katika utunzaji wa taarifa za matibabu ya wagonjwa.

Mfumo huu unarahisisha utoaji wa huduma kwa wagonjwa na upatikanaji wa taarifa kwa haraka, hivyo kuboresha huduma na kupunguza makosa katika utunzaji wa taarifa, kwani taarifa hazitunzwi kwa njia ya karatasi. Mfumo unaoungisha watumiaji kuanzia Mapokezi, Malipo, Daktari, Maabara , radiolojia, Stoo pamoja na famasi

**3. Mfumo wa Tiba Mtandao (Telemedicine)**

Hospitali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, imeanzisha mfumo wa tiba mtandao (Telemedicine) ambao unaiwezesha kutoa huduma katika hospitali za ngazi ya chini. Mfumo huu unawawezesha wataalamu wa afya kutoa huduma kwa maeneo yenye uhaba wa wataalamu, na pia unasaidia kupunguza gharama za usafiri kwa wananchi. Kwa sasa, hospitali inatoa huduma kupitia mfumo huu kwa hospitali za:

- Hospitali ya Mkoa wa Manyara
- Hospitali ya Mkoa wa Tanga
- Hospitali ya Mkoa wa Morogoro
- Hospitali ya Mkoa wa Singida

**4. Mfumo wa Kusafirisha Sampuli za Wagonjwa (Pneumatic Tube System)**

Hospitali imeanzisha mfumo maalum wa kusafirisha sampuli za wagonjwa kutoka sehemu za kutolea huduma hadi maabara kwa ajili ya vipimo. Mfumo huu unarahisisha utendaji kazi na kupunguza gharama na kuepuka muda wa muuguzi kutembea kutafuta sampuli na kupeleka maabara. Mfumo huu unahakikisha ufanisi katika huduma na kupunguza ucheleweshaji.

**5. Mfumo wa "Nursing Call"**

Hospitali inatumia mfumo wa "Nursing Call" uliowekwa katika wodi za kulaza wagonjwa. Mfumo huu unasaidia kurahisisha mawasiliano kati ya mgonjwa na muuguzi, kwani mgonjwa akiona haja ya msaada anaweza kuomba kwa urahisi kupitia mfumo huu.

# Mradi wa Mtambo wa OXYGEN
## (Oxygen Plant)






Hospitali imefanikiwa kusimika mtambo wa kuzalisha hewa tiba wenye thamani ya 1.5B. Mtambo huu una uwezo wa kuzalisha mitungi 400 ndani ya masaa 24, hivyo umekua ukiokoa gharama milioni 76 kwa mwezi na kuhudumia hospitali za jirani.



**Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano Hospitali ya Benjamin Mkapa**

